MASUALA MUHIMU YALIYOJITOKEZA WAKATI WA MAJADILIANO YA KUCHAMBUA MIPANGO NA BAJETI ZA MIKOA NA MSM 2016/17

1. Kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya akina mama na vijana asilimia 10 zinaainishwa vizuri katika mipango na bajeti kwa kuainisha Vikundi vinavyokopeshwa, Vikundi vilivyonufaika na Marejesho. Aidha Mikopo hiyo ijumuishe vikundi vya wajane.
2. Kipaumbele cha kulipa malimbikizo ya madai mbalimbali mfano walimu na uhamisho ufanyike pale tu kuna fedha za kulipa
3. Mamlaka za Serikali za Mitaa zifanye utafiti wa kutosha wa Vyanzo vya mapato na makusanyo halisi ili kupugunza mianya ya upotevu wa mapato inayosababisha mawakala kupata zaidi
4. Kudhibiti uwepo wa watumishi hewa ili kubana matumizi kwa kuweka mfumo wa ufuatiliaji utakaohusisha uhakiki kwa kuzingatia orodha ya malipo ya mishahara ya kila mwezi na kutoa taarifa katika vikao vya DCC na RCC.
5. Elimu zaidi itolewe ya matumizi ya Bima ya Afya na mifuko ya Afya ya Jamii (CHF) kwa wananchi hususani waendesha pikipiki ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma.
6. Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinakusanya kikamilifu Fedha za Ushuru wa Minara na mabango kwa kuandaa sheria ndogo na kuangalia utaratibu mzuri wa namna ya kukusanya mapato katika maeneo ambayo makampuni ya simu yanazilipa Serikali za vijiji na wananchi katika maeneo yao.
7. Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri na kusimamia kikamilifu matumizi ya mifumo ya kielekroniki na kuhakikisha zinatumika kikamilifu katika miradi iliyokusudiwa.
8. Fedha za kodi ya ardhi 30% inayotozwa na Halmashauri ziruhusiwe kukatwa moja kwa moja na Halmasauri yenyewe badala ya kusubiri kupewa na wizara ya Ardhi.
9. Msisitizo wa matumizi ya Mfumo wa kielectronic katika ukusanyaji wa mapato na kutambua vyanzo halisi wa kila chanzo na kufanya utafiti wa kina.
10. Shuru ndogo ndogo wanazotozwa wafanyabiashara wadogo na wanufaika wa TASAF ambao wanaanzisha miradi ya kujikimu

(wauza bagia, maandazi na mboga) ziondolewe ili wananchi wasisumbuliwe.

11. Halmashauri ione umuhimu wa kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ili waweze kusaidia kuhamasisha ulipaji wa Kodi na shuru mbalimbali
12. Ili kuongeza ukusanyaji wa Kodi ya Majengo kufanyike jitihada za kutambua mitaa na namba za nyumba . Mpango huu kutadhibiti ujenzi holela unaofanywa na wananchi wa maeneo hayo.
13. Halmashauri zijipange kuwa na miradi ya uvunaji wa maji ya mvua (mabwawa na malambo). Miradi hiyo pia itasaidia kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji inayosababishwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa maji.
14. Mbao zilizokamatwa na Idara ya Maliasili wanakamata zinaweza kutumika kutengeneza madawati ili kupunguza tatizo la sasa lililoloikabili nchi yetu hasa hususani katika shule ya msingi.
15. Wanahabari katika Halmashauri watumike kuzisaidia Halmashauri husika katika masuala ya kujitangaza kwa shughuli mbalimbali zinazofanyika hususani fursa za kiuchumi.
16. Fedha za Uendeshaji wa ofisi za Ma-DC zipelekwe moja kwa moja kwenye kasma husika badala ya kugawiwa na Katibu Tawala wa Mkoa
17. Kuangalia uwezekano wa Halmashauri kudhibiti risiti feki na vitendo vya rushwa zinazotolewa na wakandarasi/wazabuni kwa watumishi wa Halmashauri na kusababisha mapato mengi ya Halmashauri kupotea.
18. Gharama za upimaji viwanja ni kubwa hivyo kusababisha wananchi wengi kujenga kwenye maeneo yasiyopimwa kwa kushindwa kugharamia. Serikali iangalie uwezekano wa kuhakikisha kunakuwepo mfumo ya kuhakikisha wananchi wa Kawaida wanapata viwanja vilivyopimwa
19. Usimamizi wa sheria ndogo ya usafi wa mazingira utiliwe mkazo ili kupunguza au kuondoa kabisa milipiko ya magonjwa hususani kipindupindu
20. Ongezeko la madawati liende sambamba na ongezeko la matundu ya vyoo na Madarasa.

21. Mkakati wa kukabili ukame juhudi maalum zifanyike za kuwa na miradi mikubwa ya kuvuna maji ya mvua na kuyatumia katika miradi ya umwagiliaji na ufugaji.
22. Suala la Ushuru tokana na Majengo (Property tax) kuchukuliwa na TRA liangaliwe kwa makini ikizingatiwa kuwa rekodi za makusanyo ya mapato hayo kwa miaka ya nyuma hazikuonesha mafanikio ikilinganishwa na mafanikio ya yaliyoonyeshwa na MSM baada ya kurudishiwa ukusanyaji wa chanzo hicho.
23. Suala la Mifereji ya maji machafu kutotengenezwa na Mamlaka za Maji safi na Maji taka na kusababisha uharibifu wa barabara, hivyo kuongeza gharama za matengenezo kwa Halmashauri.
24. Majengo yote marefu ambayo hayajajenga maeneo ya ''parking'' kwa mijini yataozwe faini kwa kukiuka utaratibu ili kuongeza mapato ya Halmashauri.
25. Suala la ombaomba lishughulikiwe kwa ukamilifu, aidha wananchi waelimishwe kutowapa fedha ili waondoke mijini wenyewe kwa kuwa wanachafua mazingira ya miji.
26. TASAF III imeonekana fedha zinazotolewa zinanufaisha watu wasiowalengwa, walengwa kupewa fedha kiwango tofauti kutoka awamu moja kwenda nyingine na baadhi ya watumishi wa Serikali kunufaika. Ufuatiliaji na Uhakiki ufanyike ili kubaini fedha zilizotolewa wa wananchi wasio walengwa na watumishi wasio waaminifu. Aidha elimu itoletwe juu ya umuhimu wa fedha hizo ili kuondoa imani potovu
27. Elimu zaidi itolewe kwa wanachi juu ya faida za MKURABITA katika kuinua uchumwa wananchi na maendeleo kwa ujumla.
28. Serikali itoe vibali vya kuajiri watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususani Maafisa watendaji wa vijiji na Mitaa mabao wanaumuhimu mkubwa katika ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa shughulizi za maendeleo.
29. Fedha kutolewa kidogo na wakati mwingine kutotolewa, Serikali ione umuhimu kutoa fedha zote ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.